

Toleo La 6: Aprili - Juni 2019

Watu Mazingira

Ulimwenguni!



Kambi Ya Plover

Utalii Nyumbani

Suluhu Yatafutwa

Mzozo Wa Uvunaji Machanga Kwale

Vyakula Mwitu

Msimu Wa Mvua

Suku Ya Ndege Duniani

Tusherehekee Ndege

Kudhibiti Uvunaji Mchanga

Kukabili Kuenea Kwa Jangwa

Plastiki Marufuku!

Tanzania Yaamua

Yaliyomo

04

TAARIFA ZA MAJUKWAA

Kamati Kuu Yatupa Muktasari wa Ripoti za Robo ya Pili ya 2019 Kutoka kwa Washirikishi wa Majukwaa

05

ZIARA YA MAFUNDISHO

Taarifa ya John Safari Ziara ya Mafundisho Kaunti ya Makeni na Laikipia, Kenya Kwa Wadau wa Mradi wa Kilimo Hifadhi, Kaunti ya Kwale.

07

VYAKULA MWITU

Ruth Adeka atupa Sampuli ya Vyakula vya Kitamaduni katika Msimu wa Mvua Nchini Kenya.

09

PLASTIKI MARUFUKU!

Tanzania Yafuata Nyayo za Kenya, Rwanda na Sudan Kusini Kupiga Maruku Mifuko ya Plastiki.

11

SHEREHE ZA SIKU YA NDEGE DUNIANI

Paul Omonge Atueleza Umuhimu wa Sherehe za Siku ya Ndege wa Kuhamahama Duniani.

13

KUKABILI KUENEA KWA JANGWA

Halinishi Yusuf Atuarifu Jinsi Kaunti ya Makeni, Kenya, Inasimamia Uvunaji Mchanga Kuzuia Kuenea kwa Jangwa.

16

SULUHU YATAFUTWA

Suluhu Ya Kudumu Yatafutwa kwa Mzozo wa Uvunaji Machanga Baharini, Pwani ya Kusini mwa Kenya. Moses Ziro aripoti.

20

SIKU YA UTAFITI BAHARINI

Ripoti ya Omar Juma kuhusu Maonyesho ya Shirika la Utafiti wa Bahari na Uvuvi ya Vioto vya Kuboresha Mazingira na Chumo Riziki, Pwani ya Kenya.

22

TUZO KWA JAMII YA WASINI

Juhudi za Kikundi cha Kusimamia Fuo ya Wasini Kuregesha Upya Matumbawe Kisiwani Wasini Zatabuliwa! Abubakar Ahmed atujulisha.

23

SHEREHE ZA KASA DUNIANI

Janet Mueni Atupasha Kuhusu umuhimu wa kusherehekea Siku ya Kasa Duniani.

24

UTALII WA NYUMBANI

Kambi ya Plover Iliyoko Nyanda za Juu Nchini Kenya, ni Nyumbani kwa wanaotalii Kanda hii, kama anavyosimulia Wachira Ruhii.



Barua ya Mhariri

Karibuni kwa toleo la 6 la Jarida letu la kila robo mwaka.

Kwa miaka mingi, mchanga wa kujengea ulikuwa ni rasili mali ya bure. Kwa sasa, hali hii imebadilika. Kama ilivyo kwa mali asili nyingi, upeo wa kuvuna rasili mali hii bila malipo umefikiwa. Upeo huu haukufikiwa kwa wakati mmoja, lakini sehemu nyingi ulimwenguni umeanza kukabiliwa na uhaba wa mchanga wa kujengea. Na tumeanza kufahamu kuwa mchanga wa kujengea unazidi kuwa haba na ghali kila uchao.



**Bi. Phathisani Tabengwa,
Mhariri.**

Katika toleo hili, tumelivalia njunga swala la usimamizi wa uvunaji mchanga ili kuzuia kuenea kwa janga katika Kaunti ya Makueni, Kenya, na jinsi jamii katika kanda ya kusini mwa pwani ya Kenya wanavyo ng'ang'ana kupata suluhu kwa mzozo unaotokota baina yao na mashirika ya kiserikali kuhusu uvunaji mchanga baharini.

Mbali na taarifa hizo, tumekuandalia taarifa ya ziara ya mafundisho kwa wadau wa mradi wa kilimo hifadhi Kaunti ya Kwale, na yale waliyojifunza Kaunti ya Makueni na Isiolo, Kenya.

Kuna pia taarifa za vyakula vya kitamaduni vinavyo patikana msimu wa mvua nchini Kenya, kauli ya Serikali ya Tanzania kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, mseto wa taarifa za kuadhimishwa kwa siku muhimu za kimazingira, ikiwemo Siku ya Kasa Duniani, na taarifa nyinginezo.

Ni matumaini yangu kuwa utafurahia kusoma toleo hili la jarida letu.

Wenu,

Phathisani Tabengwa,
Bulawayo, Zimbabwe.

Taarifa za Majukwaa

Tumekuwa na shughuli chungu nzima katika majukwaa yetu katika robo ya pili ya 2019. Na tunazo habari chemchem za kuwapasha kuhusu mijadala na shughuli za majukwaa.

Jukwaa la Wanawake

(P4N Wanawake) walianza shughuli zao robo hii kwa kuandaa uchaguzi wa Mshirikishi Mwenza. Bi. Ashengai Kimath, aliweza kuchaguliwa Mshirikishi Mwenza wa kwanza wa jukwaa hili. Yeye ni muanzilishi wa shirika la Environmental Action and Community Development, lenye ofisi mjini Arusha, Tanzania. Bi. Ashengai ana Shahada ya Geografia na Mazingira (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), na ya Uzamili katika Usimamizi wa Elimu na Uongozi (Chuo Kikuu cha Arusha).

Jukwaa la P4N Wanawake waliweza kujadili wasifu wa kiongozi shupavu anayeweza kuigwa na viongozi wanawake. Kwa kauli moja, jukwaa walikubaliana kuwa kiongozi shupavu lazima atoe muelekeo muafaka, awatie moyo wafuasi wake, mjasiri, mpenda kazi yake, aliyejitolea na mwenye maono makubwa. Jukwaa pia lilitoa mwito wa

kuwaiga mama zetu, waliokuwa na uwezo wa kutumia rasili mali kidogo kulisha jamii nzima. Jukwaa la Misitu na Wanyama Pori liliangalia upya Mkakati wa Upanzi wa Miti kufuatia changamoto zilizo kabili wanachama walipoanza kuutekeleza. Kwa sasa mkakati umeboreshwa na kutoa muongozo wa kutambua wanaoweza saidiwa kuendeleza bustani za miche, usimamizi wa miche itakayo pandwa na soko.

Jukwaa la Vijana liljadili kwa kina mipango ya kuanzisha vilabu vya vijana katika shule na vyuo. Jukwaa liliamua kuwa wasimamizi wa shule wangeweza kushauriwa kuanzisha vilabu hivi kwenye shule zisizo na vilabu vya mazingira. Baadhi ya shughuli za vilabi hivi zitakuwa upanzi wa miti, mashindano ya uchoraji, nyimbo, na shughuli nyinginezo za kimazingira. Katika robo hii, Shule ya Msingi ya Utange, Kaunti ya Mombasa, Kenya,

ilikuwa ya kwanza kuanzisha klabu cha vijana waWatu Mazingira. Mwalimu, Bi. Elizabeth Kadzo (P4N-210), ndiye msimamizi wao. Klabu hiki kina wanachama 20.

Majukwaa mengine yako katika harakati za kumaliza mijadala yao. Jukwaa la Jamii Asili linatengeza mkakati wao wa mawasiliano, Jukwaa la Maji wanajadili mbinu za uvunaji endelevu wa mchanga, Jukwaa la Biashara Mazingira linatengeneza miundo bora ya biashara endelevu ya utalii pwani, Jukwaa la Kilimo Hifadhi na Uvuvi

linajadili mikakati ya kukuza uvuvi, ili hali Jukwaa la Elimu na Hamasisho lilichukua muda wao mwingi kuboresha jarida letu.



**Bw. Silvanus Uunona,
Mwenyekiti, Watu Mazingira Ulimwenguni.**



Washikadau wakionyeshwa jembe la kuvutwa na tingatinga katika Kituo cha Huduma za Vifaa vya Kilimo, Wote, Kaunti ya Makueni, Kenya.

ZIARA YA MAFUNDISHO MAKUENI NA LAIKIPIA

Baada ya zaidi ya miaka mitatu ya utekelezaji wa mradi wa Kilimo Hifadhi ulio fadhiliwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO), washikadau wa mradi huu walitembelea Kaunti za Makueni na Laikipia, kuanzia tarehe 28 Aprili hadi Mei 4, 2019. Jumla ya wakulima, watoa huduma na maafisa wa Serikali 26 walijumuishwa katika ziara hii.

Ziara hii ilikuwa muhimu kwa washikadau ili kuwapa fursa ya kujifunza kuhusu mbinu bora za kilimo hifadhi katika Kaunti hizi. Washikadau pia walikuwa na hamu ya kujua vifaa mbalimbali vya kilimo vinavyo tumiwa na wakulima, na jinsi wanavyo kusanya na kuuza mazao yao.

Kaunti ya Makueni

Ziara ilianza Kaunti ya Makueni. Kaunti ya Makueni ni moja ya Kaunti kame nchini Kenya. Baadhi ya shughuli kuu za kilimo katika Kaunti hii ni ukuzaji wa maembe, pojo, nyanya, makonge, pamba, na nafaka. Mradi wa Kilimo Hifadhi umeungwa mkono na Serikali ya Kaunti ya Makueni na wakaazi kwa jumla.

Ufanisi wa matumizi ya mbinu bora za kilimo hifadhi umefanya watoa huduma wa kutayarisha mashamba kuanza kutumia mitandao ya kijamii ili kuweza kuwa hudumia wakulima kwa urahisi.

Baada ya kutembelea ofisi kadhaa za Serikali ya Kaunti, washikadau walitembelea Kibwezi East Cooperative Society. Shirika hili lina wakulima wanachama 600 wanaokuza nafaka, Tingatinga na majembe yanayovutwa na ng'ombe hutumiwa kulima mashamba, na maji ya kunyunyizia mashamba hupatikana Mto Athi. Kwa sasa, wakulima huvuna magunia 6 (kilo 90/gunia) kwa eka.

Baadaye, washikadau waliweza kutembelea Kijiji cha Wakulima wa Biashara cha Kiteng'ai. Kikundi hiki kilianzishwa 2010 ili kutosheleza Wadi ya Mtito Andei kwa chakula. Kikundi kina wakulima 150 walio pewa kandarasi na kampuni ya Imara kukuza nafaka.

Kikundi kina mikakati mizuri ya usimamizi. Kuna kamati za uzalishaji, mauzo, ubora wa bidhaa na hata kamati ya akiba na mikopo.



Washikadau wakiwa katika Kituo cha Huduma za Vifaa vya Kilimo cha Kaunti ya Makueni, mjini Wote.

Mpango wa akiba na mikopo ulianzishwa na Gavana wa Makueni, Prof. Kivutha Kibwana, baada ya wakulima kumsihi kufanya hivyo.

Kikundi kinajivunia kuwa na kandarasi za uzalishaji na kampuni ya mbegu ya Dean (2011); kununua kiwanja; kuhakikisha vikundi wanachama 22 wana vifaa vya ukulima; na wakulima wanajitosheleza kwa chakula, fedha na wanauwezo wa kutafuta mikopo kwa gharama ndogo. Serikali ya Kaunti ya Makueni pia imewanunulia tingatinga mbili kusaidia katika shughuli za kilimo.

Kutoweza kufikia kiwango cha uzalishaji na ubora wa bidhaa wanazokuza kwa kandarasi, kuchelewa kwa malipo, na uharibifu wa wadudu kwa mazao ni baadhi ya changamoto wanazo zikumba.

Kaunti ya Laikipia

Laikipia pia ni Kaunti kame inayo patikana upande mkavu wa mlima Kenya. Kilimo kukubwa katika Kaunti ni cha mahindi, ngano, maharagwe na viazi. Wakulima wengi, wakiwemo wakulima wa mashamba makubwa, wameanza

kutumia mbinu za kilimo hifadhi ili kupunguza gharama za ukuzaji, kuboresha rotuba ya udongo na kwa usimamizi endelevu wa mali asili.

Serikali ya Kaunti imenunua tingatinga 5, zenye uwezo wa kuvuta majembe na vipandio, ili kusaidia mradi wa Kilimo Hifadhi.

Katika Kaunti ya Laikipia, washikadau walimtembelea Bw. Duncan Macharia, mtoa huduma za kulima mashamba. Huduma hii aliianzisha 1980 akitumia vifaa vya kuvutwa na ngombe. Lakini baada ya kupata elimu kutoka kwa mradi wa Kilimo Hifadhi, aliacha kutumia ng'ombe na kununua tingatinga, ili kumudu mahitaji ya wakulima na kuondoa wasiwasi wa kutokuwa na nyasi kwa ng'ombe wakati wa kiangazi.

Tingatinga linasaidia kupunguza gharama ikilinganishwa na mbinu za kawaida za kulima na kupanda. Tingatinga linaweza kuunganishwa na mashini ya kupukusa mahindi, mashini ya kupiga maji, jembe la kulima na bomba la kunyunyizia dawa. Uwekaji rekodi nzuri na uaminifu kwa wateja, ni baadhi ya mambo yanayo muwezesha kukuza biashara yake.

Washika dau pia walipata fursa ya kutembelea Kikundi cha Chakula Tele, kijijini Male. Hapa waliweza kujionea shamba lenye mpangilio bora, uvunaji wa maji, uhifadhi wa unyevu wa udongo kutumia mimea, shamba la maonyesho, ufugaji wa nyuki, shamba la maboga, vifaa vya kilimo hifadhi na ufugaji wa ngombe katika zizi.

Mpangilio wa matumizi ya shamba, kuweko kwa bei sawa za watoa huduma, ukuzaji kwa kandarasi ni baadhi ya mambo ambayo washikadau walijifunza na kamua kuzingatia.



Bw. John Safari (Muandishi wa Makala) ni Msaidizi wa Mkurugenzi wa Kilimo Kaunti ya Kwale (Mimea) na Mwakilishi wa Nyanjani wa FAO, Kaunti ya Kwale.

VYAKULA MWITU

Bí. Ruth Adeka, wa Shirika la Makavazi Kenya, Atuarifu kuhusu vyakula vya Msimu wa Mvua.

Kenya inajulikana kwa utajiri wa bio-anuai, ikiwemo wanyama na mimea wanaopatikana katika maeneo mbalimbali kuanzia nyanda za juu zenye baridi hadi nyanda za chini zenye joto. Kenya pia ina utajiri wa tamaduni na vyakula vya kitamaduni mabalimbali kutoka kwa jamii wanaopatikana nchini Kenya.

Vyakula vimekuwa moja ya tamaduni za watu wa Kenya kwa karne nyingi. Vyakula kama mboga, matunda, viazi, mahindi na njugu zinakuzwa ama kukusanywa kutoka mwituni. Vyakula vingine ni kama vyoga, wadudu, mabuu, konokono, ndege na vyakula vingine vinavyoliwa na binadamu.

Uwepo wa vyakula nchini Kenya hutegemea sana misimu. Kuna misimu miwili ya mvua kwa mwaka, msimu wa masika, kuanzia Machi hadi Aprili, na msimu wa vuli, kuanzia Oktoba hadi Disemba. Majira hayo mengine kuna vipindi vya jua.

Mvua huja na baraka tele. Mboga za kitamaduni, wadudu wanaoliwa na vyoga hupatika kwa wingi na kuwapa biandamu lische bora. Baadhi ya mboga zinazo patikana misimu ya mvua ni: -

1. Kongwa

Hujulikana pia kama dzadza (Giriama), iinyororo (Maragoli), mukengeria (Kikuyu), odielo (Luo), ama common yellow commelina (Kiingereza), Commelina Africana (Kisayansi).

Hupatikana mwanzo mwanzo wa msimu wa mvua kabla mboga nyingine hazijafikia kiwango cha kuvunwa. Kongwa ni mboga nyororo na huchanganywa na mboga nyingine wakati wa kupika. Ni kitoweo kwa jamii ya Luhya, Teso, Mbeere na Luo.

2. Togotia (Kikuyu)

Enyaro (Maa), gamba (Taita), *Erucastrum arabicum*, (kikisayansi), hupatikana kwa wingi msimu wa mvua mjini

Nairobi na nyanda za juu magharibi na mashariki mwa Bonde la Ufa, hasa kwenye vijito. Mboga hizi huchanganywa na mukimo, chakula kilichopendwa kanda za kati mwa Kenya. Ni chakula pia kwa jamii ya Kipsigis na Kamba.

3. Logatsi (Mijikenda)

Amaranthus graecizans, (kisayansi) ama pigweed (Kiingereza), hupatikana katika sehemu zisizo na mvua ya kutosha na katika maeneo lowevu kama gugu. Ni chakula kitamu kushinda mboga zingine katika familia hii, hasa ikiwa kitoweo kwa ugali ama kubondwa na kuchanganywa na mahindi na maharagwe.



Viazi vya kuchemsha pamoja na Logatsi kama kitoweo.

Vyoga Vinavyoliwa

Vyoga vyatambulika kama mimea, lakini viko katika kundi la kuvu (fungi). Vyoga vina wingi wa protini, vitamini B na madini yenye nguvu ya kuzuia kuharibika kwa chembechembe za mwili. Vyoga pia husaidia moyo kwa kusafisha na kuthibiti kasi ya damu.

Vyoga hupatikana mwituni wakati wote wa msimu wa mvua. Katika kanda ya pwani, hupatikana vikikua katika miti kama mrihi, mbuyu unaozua na hata vichuguu. Aina ya vyoga vinavyoliwa ni kama vile vyoga udzondo, vyoga muyu, vyoga nyama, vyoga mamewe, uhovu, vyoga rerema, vyoga sikiro, vyoga mkundu wa nyani, vyoga mbwate na vinginevyo. Vyoga mamewe ndio vikubwa zaidi na vinaweza kufika ukubwa wa uteo.

Vyoga ambavyo haviliwi na jongoo huwa vina sumu kwa binadamu.

Vyoga kwa kawaida hupikwa kwa kuviosha vizuri na kuvichemsha na viungo kama vile embe bichi lililio katwakatwa, rojorojo la mabuyu kuongeza chachu na hata tuwi la nazi.

Unaweza pia kuvichoma kwa moto na kula.

Wadudu Wanaoliwa

1. Mchwa, ama lutwa (Giriama), tsitswa (Luhya), hutoka nje majira ya jioni wakati wa mvua. Hushikwa kwa kuchimba shimo na kuweka mwangaza kando yake. Ndoo yenye maji huwekwa karibu na mwangaza na wakati mchwa

wanapofuata mwangaza, mabawa yake hulowa na maji na kushindwa kuruka. Mchwa huuzwa sokoni. Hupikwa kwa kuwaosha, kuwaweka kwa kikarango moto ili kuondoa mabawa na kuongeza chumvi ili kuleta ladha. Mchwa wana wingi wa protini.

2. Chenene ni rangi ya kahawia na huishi ndani ya udongo. Watoto huchimba mashimo ili kuwatoa na kuwapeleka nyumbani. Chenene anaweza kukuuma na miguu yake ina miba inayoweza



Chenene

kudhuru mtu.

3. Viwavi huishi kwa miembe, mikoroshu na miti mingineyo. Huliwa wakiwa viwavi kabla wabadilike kuwa vipepeo. Hupatikana msimu wa mvua (Aprili) wakati majani machanga hupatikana kwa wingi. Viwavi hukamuliwa ili kutoa yaliyomo kwa utumbo na kukata sehemu ya mwisho wa mwili. Hukarangwa na kuongezwa chumvi, tayari kwa kula.

PLASTIKI MARUFUKU!

Serikali ya Tanzania imepiga marufuku mifuko ya plastiki inayotumika mara moja tu ili kukabiliana na uchafuzi wa plastiki. Kulingana na Kanuni za Mifuko ya Plastiki 2019, kuagiza, kuuza kwa masoko ya kimataifa, utengenezaji, mauzo, uhifadhi, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki bila kujali unene wake umepigwa marufuku.



Kanuni mpya zilianza kutekelezwa Tanzania bara kuanzia Juni 1, 2019. Kanuni hizi, hata hivyo, hazitatumika kwa plastiki zinazotumika kwa huduma za matibabu, bidhaa za viwanda, tasnia ya ujenzi, sekta ya kilimo, vyakula, na usimamizi wa usafi na taka.

Taarifa Kutoka kwa Ofisi ya Katibu

Wasafiri wanaoingia Tanzania wametahadharishwa, kupitia taarifa kwa wasafiri iliyotolewa Mei 15, 2019, kutobeba mifuko ya plastiki wanapoanza safari ya kwenda Tanzania. Tahadhari hii pia imewaarifu wasafiri kuwa mifuko inayotumiwa kupakia bidhaa za chooni zitaruhusiwa.

Safari ya kupiga marufuku plastiki ilianza Agosti 2016, wakati serikali ilipo waonya wazalishaji wa mifuko ya plastiki kutafuta mbadala wa plastiki katika biashara yao ili kujitayarisha kwa marufuku ya mifuko ya plastiki iliyo pangwa.

Tanzania sasa imejiunga na Kenya, Rwanda na Sudan Kusini katika kupiga marufuku mifuko ya plastiki. Sio nchi nyingi zimeweza kufaulu kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Uganda, kwa mfano, ilipiga marufuku mifuko nyembamba ya plastiki 2007. Lakini amri haikukelezwa.

Kukiuka kanuni hizi kuna kifungo cha miaka miwili jela au faini ya hadi Tshs. 1 bilioni, ilihali yeyote atakaye patikana akitumia mifuko ya plastiki anaweza tozwa hadi Tshs. 200,000 ama kifungo cha hadi siku 7, ama adhabu zote mbili.

Wazalishaji wa mifuko ya plastiki wameanza kuzalisha mifuko mbadala ili kukimu mahitaji ya mifuko.

*Tanzania Yafuata
Nyayo Za Kenya,
Rwanda Na Sudan
Kusini Kupiga
Marufuku Mifuko
Ya Plastiki.*

Waziri katika ofisi ya Naibu wa Rais anaye husika na maswala ya Mazingira, Bw. Januari Makamba, amewahakikishia wana biashara kuwa serikali ina mipango ya kuwezesha wazalishaji wa mifuko mbadala kwa kuweka viwango, sheria na kanuni mpya.

'Serikali itaendelea kuwasaidia wazalishaji wa mifuko mbadala ili kuhakikisha hakutakuwa na upungufu wowote. Pia tunawashukuru wananchi kwa kuitikia mwito na kufanya kampeni ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki kufaulu,' Waziri akanukuliwa akisema.

Uchunguzi wetu, kati ya wanachama wetu nchini Tanzania, umebaini kuwa wananchi wengi wamepokea vizuri marufuku hii na wameanza maisha mapya bila mifuko ya plastiki.

Bw. Kusundwa Wamalwa, akiwa Katavi, ameona kuwa kuna makundi matatu ya wananchi walioathiriwa na marufuku hii. Kundi la kwanza ni la wana biashara waliokosa muda wa kutosha kuuza mali waliyo kuwa nayo na kulazimika kuitupa.

Kundi la pili ni la wananchi wa kawaida wanaotumia mifuko ya plastiki kwa shughuli zao za kila siku. Hawa walilalamika kuwa hawakupewa muda wa kutosha kujitayarisha, na mwanzoni walilazimika kutumia magazeti ama

mifuko ambayo ilikuwa ghali na ya ubora wa chini. Na kundi la tatu ni la waliokuwa na ufahamu wa madhara ya plastiki, walio shangilia wakati marufuku ilipo tangazwa.



Sampuli ya mifuko mbadala inayo pendekezwa

Bw. Kusundwa ni mmoja wa wale walio shangilia marufuku ya 'rambo', kama mifuko ya plastiki


inavyo julikana nchini Tanzania. Alipoulizwa, Bw. Frank Maro, (Mweka Hazina, Watu Mazingira Ulimwenguni), akiwa Mwanza, alisema kuwa wananchi walielewa madhumuni ya serikali na kukubali marufuku hiyo. Bi. Ashengai Kimanth (Mshirikishi Mwenza, Jukwaa la Wanawake) na Bi. Martha Ntoipo, wakiwa Arusha, walikuwa na mtazamo sawia.

Lakini Bi. Rashida Zaid, akiwa Arusha, aliona kuwa, ijapo wananchi wameunga mkono serikali kupiga marufuku mifuko ya plastiki, mifuko mbadala iko ghali.

Kulingana na shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, nusu ya plastiki zinazozalishwa ulimwenguni, zimeundwa kutumika tu mara moja na kutupwa. Kwa miongo kadhaa, plastiki hizi zimechafua bahari na nchi kavu kwa kasi sana, na kuhatarisha maisha ya binadamu na wanyama.

Serikali inaamini kuwa hii ni hatua ambayo lazima ichukuliwe ili kutengeneza mazingira mazuri na safi.

Siku ya Ndege Duniani!



Bw. Paul Omonge, muandishi wa makala, ni mwanafunzi wa Uzamifu, Chuo Kikuu cha Mali Asili na Sayansi ya Maisha, Vienna, Austria.

Kauli mbiu ya sherehe za Siku ya Ndege wa Kuhamahama Duniani 2019 ni “**Linda Ndege: Kuwa Suluhu kwa Uchafuzi wa Plastiki!**”

Kuna Umuhimu wa Kusherehekea Siku Hii?

Kuhamahama kwa ndege kutoka sehemu moja ya dunia hadi nyingine ni moja ya matukio ambayo yametubumbuaza. Ijapo viumbe wengi huhama, kuhama kwa ndege huvutia kwa vile safari yao huwa ndefu na hupitia bara moja hadi nyingine.

Kuna aina 11,000 za ndege duniani, na kati ya 5, mmoja ni ndege wa kuhamahama. Kati ya hawa, 40% wameendelea kupungua kwa idadi, na kati ya 8, mmoja yuko katika tisho la kuangamia duniani. Kwa hivyo, siku hii ni ya kampeni ya kuhamasisha umma kuhusu changamoto zinazo wakumba ndege wa kuhamahama ulimwenguni na haja ya kuhifadhi makao yao.

Sherehe hizi pia hutumiwa kuisisitiza umuhimu wa ndege kwa ikolojia na haja ya ushirikiano wa kimataifa ili kuhifadhi ndege na makao yao. Kozi-Kipanga (Peregrine Falcon), Mbayuwayu wa Bluu (Blue Swallow), Shakwe wa Aktiki (Arctic Tern), Polohoyo (European Bee Eater), Bata Bukini wa Misri (Egyptian Goose), ni baadhi ya ndege wa kuhahama.

Tishio Kwa Ndege

Uchafuzi wa plastiki ni tishio kubwa kwa ndege, kama ilivyonukuliwa katika kauli mbui za sherehe za mwaka huu. Baadhi ya tishio nyingine ni kama kupotea ama kuharibiwa kwa makazi yao kutokana na upanuzi wa kilimo, nyaya za stima, tabo za upepo, uwindaji haramu na uuaji wa ndege.

Sumu zinazotumiwa na wakulima kuzuia ndege kula mimea shambani huathiri sana ndege wa kuhahama. Kwa kuongezea, mabadiliko ya mfumo wa hali ya hewa umeathiri kuhama kwa ndege.

Juhudu za Kimataifa za Kuhifadhi Ndege

Mkataba wa Uhifadhi wa Spishi za Kuhama za Wanyama Mwitu, ijulikanayo pia kama Mkataba wa Bonn, na Makubaliano ya Afrika, Uropa na Asia kuhusu Uhifadhi wa Ndege wa Majini wa Kuhamahama, ni makubaliano yanayo tumiwa kuongoza uhifadhi wa ndege wa kuhamahama. Nature Kenya, Shirika la Makavazi Kenya na Shirika la Wanyama Pori Kenya, ni baadhi ya mashirika yanayo andaa sherehe hizi mashinani, wakishirikiana na wadau wengine.

Shughuli za Kuadhimisha Siku Hii

Miaka michache iliyopita, niliungana na wenzangu kuandaa sherehe za kuadhimisha siku hii katika fuo ya Dunga, Kisumu, katika ziwa Victoria, Kenya. Tuliandaa mashindano ya mashua, hotuba na tuzo kwa wanafunzi walio tumbuiza wageni kwa nyimbo, mashairi na michezo ya kuigiza kuambatana na kauli mbiu. Vikundi vya kijamii,

12

shule na idara za serikali walihudhuria sherehe hizi. Wasimamizi wa Fuo ya Dunga, Kikundi cha Utalii Mazingira cha Vijana wa Dunga, pamoja na Muungano wa Waelekezi wa Safari za Watalii wa Ziwa Victoria walihudhuria.

sherehe hizi kote ulimwenguni wakati ndege hawa wanapo hama. Mwaka huu sherehe zitakuwa Mei 11 na Oktoba 12.

Sherehe hizi kuandaliwa sehemu mbali mbali duniani zikiongozwa na kampeni na lengo moja. Wale ambao wangependa kuandaa



Sherehe za Ndege wa Kuhamahama, katika Ziwa Elementaita, Bonde la Ufa, Kenya.

Mipangilio

Kuanzia 2018, Siku ya Ndege wa Kuhamahama Duniani imefanywa tukio la kila mwaka, na kusherehekewa kila Jumamosi ya pili ya Mei na Oktoba. Jambo hili limerahisisha maandalizi ya

Watu Mazingira, Ulimwenguni!

sherehe hizi wanaweza kusajili mipango yao kutumia kiunganishi <http://www.worldmigratorybirdday.org/participate> ama kusambaza kwa mitandao ya kijamii kutumia **#WorldMigratoryBirdDay**.

KUKABILIANA NA KUENEA KWA JANGWA

Ukame, ukataji miti kiholela na matumizi mabaya ya ardhi kumechangia kuenea kwa jangwa ulimwenguni. Takriban asili mia 20 ya ardhi duniani iko katika hatari ya kuwa jangwa na kuathiri uchumi, mazingira na hata kuhamisha watu. Kuenea kwa jangwa na ukame ni mambo yanayo husiana, na tusipo chunga,



**Bi. Halinishi Yusuf,
(Muandishi wa Makala)
ni Mkurugenzi Msimamizi,
Halmashauri ya Uhifadhi na
Matumizi ya Mchanga, Kaunti ya
Makueni.**

yanaweza kuwa changamoto kwa maendeleo endelevu, hasa kwa nchi zinazostawi.

Tunahitaji kuweka desturi bora za usimamizi wa ardhi na maji, pamoja na sera zinazo kuza mazingira endelevu ili kukabiliana na kuenea kwa jangwa. Ni muhimu tujitahidi kuzuia kuenea kwa jangwa kwa sababu kuna gharama kubwa kuregesha upya maeneo ya jangwa, na matokeao yake si ya kuridhisha. Utafiti unaonyesha kuwa ifikapo 2050, watu bilioni 1.8 wata athiriwa na uhaba mkubwa wa maji, na thuluthi mbili za dunia zitakuwa na uhaba wa maji.

Jinsi ambavyo idadi ya watu inavyo ongezekwa, hasa maeneo kavu, ardhi zaidi

itazidi kudhoofika, na hii itazidisha athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Mseto wa usimamizi wa ardhi na maji ndio njia bora ya kukabiliana na kuenea kwa janga. Kuzuia mrundiko wa chumvi kwa udongo na njia nyinginezo za kulinda udongo usizorote, inaweza kuwa njia mwafaka wa kuzuia kuenea kwa jangwa.

**Siku ya Kukabiliana na
Kuenea kwa Jangwa
Duniani husherehekewa
kila mwaka tarehe 17
Juni.**

**Ni siku ambayo
imeadhimishwa tangu
1995 kwa lengo la
kuhamasisha umma
kuhusu juhudi za
kimataifa ili kukabiliana
na kuenea kwa jangwa na
athari za ukame.**

**Sherehe za kitaifa
ziliadhimishwa Makindu,
Kaunti ya Makueni,
Kenya. Kauli mbiu ya 2019
ilikuwa “Tutayarishe Siku
za Usoni Pamoja”.**

Mbinu bora za usimamizi hujumuisha miundo ya kilimo mseto, mbinu ya jadi ya kupunguza kasi ya mtiririko wa maji kwa kupanda miti, na kupunguza mmomonyoko wa udongo. Kulinda misitu ni njia muhimu ya kuzuia kuenea kwa jangwa na hasa kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokana na upepo na Kasi ya maji.

Kwa sehemu kame kama Kaunti ya Makueni, uvunaji mchanga kiholela kumechangia pa kubwa kwa kuenea kwa jangwa.

Ndani ya miongo miwili, uvunaji mchanga umeongezeka mara dufu, kama ilivyo katika Kaunti kame kama Kajiado, Makueni na Machakos, kwa sababu ya mahitaji makubwa ya mchanga wa kujengea kutoka kwa mito.

Ukaribu wa Kaunti hizi na jiji la Nairobi, ujenzi wa reli ya kisasa na miradi mikubwa ya ujenzi,



Lori la kubeba mchanga tayari kusafirisha bidhaa hiyo kutoka kwa moja ya bonde la mto mkavu, katika Kaunti ya Makueni.

kumeongeza mahitaji ya mchanga kutoka mitoni.

Kutokana na ukosefu wa kanuni, uvunaji mchanga umekuwa ukifanywa bila kuzingatia athari zake kwa mazingira, uwepo wa maji, na jinsi wakazi wanavyo jikimu kimaisha katika maeneo haya. Matokeo yake yamekuwa uharibifu mkubwa wa mito na uwezo wake wa kuhifadhi maji, na kupelekea upungufu wa maji chini ya ardhi.

Hii inadhihirishwa na vile mito inakauka haraka baada ya mvua kuisha na kukauka kwa visima.

Hatima yake imekuwa ukosefu wa maji unao athiri shughuli za kilimo, ongezeko la umbali wa kupata maji na wakati unaopotezwa kutafuta maji, kuangamia kwa viumbe vya majini, upungufu wa mimea na miti, na hata kuongeza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Baada ya kuona athari za uvunaji mchanga kiholela, Serikali ya Kaunti ya Makueni ilipitisha sheria ya Uhifadhi na Matumizi ya Mchanga 2015, iliyotoa mwongozo wa uhifadhi na matumizi endelevu ya mchanga. Sheria hii pia iliwezesha kuundwa kwa

kuzuia usafirishaji wa mchanga nje ya kaunti na kusimamia uvunaji kwa mahitaji ya kaunti ili kuhakikisha uvunaji endelevu.

Usimamizi wa shughuli za uvunaji mchanga umetoka katika enzi za mizozo na fujo

Kulingana na ripoti moja ya Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (2019), yenye kichwa “Mchanga na Uendelevu: Suluhu Mpya kwa Usimamizi wa Mazingira ya Rasilimali ya Mchanga Ulimwenguni”, imearifua kuwa mchanga ni rasilimali inayovunwa zaidi, baada ya maji, na isiyo na usimamizi mzuri ulimwenguni. Ripoti hii imependekeza umuhimu wa kanuni za kusimamia uvunaji mchanga kuhakikisha matumizi endelevu.

Kaunti ya Makueni imekuwa mfano mzuri wa eneo ambalo uvunaji mchanga kiholela ulichangia kuenea kwa jangwa na hatimaye kuundwa kwa sheria za uhifadhi na matumizi ya mchanga. Sheria inasaidia kuthibiti uvunaji mchanga kiholela, kuenea kwa jangwa na hata kupunguza makali ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa Kaunti kama kama Makueni.



Moja ya mito katika Kaunti ya Makueni ambayo haija athiriwa na uvunaji kiholela wa mchanga.

halmashauri iliyopewa mamlaka ya kuongoza shughuli za uhifadhi na matumizi endelevu ya mchanga katika Kaunti ya Makueni.

Ndani ya miaka minne tangu sheria hii kupitishwa, utaratibu muafaka umewekwa wa kuvuna mchanga ikiwemo

na kuingia katika usimamizi unaozingatia uhifadhi na uvunaji endelevu kama ilivyo elekezwa na sheria.

Kutokana na haya, visima na mito ambayo ilikuwa imekauka sasa imeanza kurudi upya na kuwezesha unyunyiziaji mdogo wa mashamba, kutokana na maji zaidi kubaki chini ya ardhi.

SULUHU YATAFUTWA!

Mzozo wa Uvunaji Mchanga Baharini, Kusini mwa Pwani ya Kenya.

Halmashauri ya Bandari za Kenya ina malengo makuu ya kupanua bandari ya Mombasa na kuifanya bandari kubwa zaidi kanda hii ya Afrika. Mpango wa upanuzi umegawanywa katika awamu tatu zikilenga kuongeza sehemu za kupakulia mizigo. Mradi huu ukifaulu, utakuwa na manufaa makubwa kwa taifa la Kenya.

Mradi wa upanuzi wa bandari utahitaji mita

mchemraba 15.5 milioni za mchanga. Kwa sasa, awamu ya kwanza imeisha na mita mchemraba 7.5 milioni za mchanga zishatumika.

Ni wakati awamu ya pili ilipoanza, ndipo Halmashauri

ya Bandari ilipogundua kuwa mchanga katika fuo ya Shella na kilangobahari cha Kilindini zilizotambuliwa awali kwa uvunaji wa mchanga, hazingeweza kutosheleza mahitaji yaliyo lengwa.



Maandamano katika Fuo ya Kongo, Diani, Kaunti ya Kwale, dhidi ya uvunaji mchanga baharini.

Kulikuwa na uhitaji wa kutafuta sehemu mbadala.

Katika Kaunti ya Kwale, kusini mwa Kaunti ya Mombasa, mchanga mwingi ulipatikana ufuoni na baharini. Kuweza kuvuna mchanga sehemu hii,

Halmashauri ya Bandari ilihitajika kufanya utathmini wa athari za mradi kwa mazingira ya bahari na jamii wanaotegemea mazingira haya, kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2015.

Utathmini huu, pia, ungependekeza mikakati ya kukabiliana na athari za mradi ambazo zingetokea. Utathmini huu hufanywa kwa mradi wowote ule ambao unakisiwa unaweza kuwa na athari kubwa kwa mazingira au jamii, bila kujali ukubwa wa mradi wenyewe.

Washikadua walihusishwa katika tathmini ya uvunaji mchanga uliofanywa na Halmashauri ya Bandari katika Kaunti ya Mombasa na kukubaliana na ripoti hiyo, kabla uvunaji kuanza.

Utaratibu huu, hata hivyo, haukufanywa kabla uvunaji mchanga kuanza Machi 2019 katika bahari ya Waa na Tiwi, Kaunti ya Kwale.

Si mara ya kwanza mrradi mkubwa wa kimaendeleo umelenga Kaunti ya Kwale kwa uvunaji wa mchanga. Mnamo Julai 2015, Mahakama ya Mazingira nchini Kenya, ilisimamisha Shirika la Reli la Kenya na Shirika la Madaraja na Barabara la China, kuvuna mchanga katika bahari ya Kaunti ya Kwale ili kujenga reli ya kisasa nchini Kenya.

Kwa sasa, uvunaji wa mchanga unafanywa na **Wihelm van Oranje**, meli inayomilikiwa na Boskalis, kampuni ya Uholanzi iliyopewa kandarasi na kampuni ya Toyo ya Ujapani kwa ujenzi wa awamu ya pili ya bandari. Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la Uhusiano wa Kimataifa wa Japani (JICA).

Wakaazi wa Kaunti ya Kwale, pamoja na washikadau wengine, wametoa kilio chao kuhusu athari za oparesheni ya uvunaji mchanga unaoendelea baharini. Wavuvi ndio wa kwanza kuona athari hizi.

Vumbi na misukosuko katika

mchanga wa fuo za Tiwi na Diani umeanza kuonekana, na mchanga kuelekea baharini kuziba timbo zilizo wazi ndani ya bahari baada ya kuvunwa mchanga.

Washikadau Watafuta Suluhu

Amri ya kusitisha uvunaji



Moses Ziro (kushoto), Mwandishi wa Makala, akiwa na wenzake wawakilishi wa Mwavuli wa Kitaifa wa Mashirika ya Kimazingira nchini Kenya, (NECSA-K) walipotembelea Fuo ya Kongo, Diani.

mazingira ya bahari kutokana na uvunaji mchanga umeharibu maeneo ya kuvulia samaki na mazalio ya samaki, na kua samaki, matumbawe na viumbe vingine hai baharini. Na kwa siku za hivi karibuni, mmomonyoko wa

mchanga ilitolewa baada ya kilio cha washikadau na Waziri wa Usafiri, Miundombinu, Nyumba na Maendeleo ya Miji, tarehe 26 Machi 2019, ili kutoa fursa kwa Halmashauri ya Bandari kushauriana na washikadau.



Wawakilishi wa KCNRN, Serikali ya Kaunti ya Kwale na NECSA-K walipo kutana na Bw. Christopher Obure, Katibu katika Wizara ya Usafiri, Miundombinu, Nyumba na Maendeleo ya Miji, ofisini kwake, Nairobi.

Mpango wa kuunda mikakati ya fidia kwa wavuvi katika Kaunti ya Kwale, ulioanzishwa na Halmashauri ya Bandari, umezua utata baada ya wavuvi na washikadau wengine kuzua hofu kuwa mchakato huu umetenga sehemu kubwa ya washikadau.

Kamati Maalum ya Bunge kuhusu Mazingira, ilifanya kikao na washikadau Ukunda, Kaunti ya Kwale, tarehe 4 Mei 2019, kufuatia mualiko wa Halmashauri ya Bandari. Washikadau walikuwa na matumaini kuwa maamuzi jasiri

yangeweza kuchukuliwa kutatua mzozo huu, ikiwemo kusitisha uvunaji mchanga kwa muda hadi pale sugu muafaka itakapo patikana. Jambo hili halikutokea.

Ni baada ya ziara ya Kamati Maalum ya Bunge kuhusu Mazingira ambapo Kwale County Natural Resources Network (KCNRN), mwavuli wa mashirika ya kijamii Kaunti ya Kwale, walipoamua kupeleka malalamishi ya jamii ya Kaunti ya Kwale kwa Serikali ya Kitaifa, Nairobi.

Ilikuwa imebainika wazi kuwa kutokuwepo kwa ripoti ya utathmini wa athari za mradi kwa mazingira na kwa jamii ndio ilikuwa kiini kikubwa cha mzozo. Ripoti hii ingetoa muongozo wa jinsi mazingira yange regeshwa upya pamoja na mpango wa fidia kwa jamii watakaopoteza chumo riziki zao.

KCNRN, wakishirikiana na NECSA-K, walikusanya mapendekezo ya washikadau ya kumaliza mzozo.

Mapendekezo yaliyokusanywa ni: -

1. Kusitishwa mara moja kwa oparesheni ya kuvunaji mchanga baharini kutoa nafasi ya tathmini kamilifu kufanywa,
2. Kusitishwa mara moja kwa mchakato wa kupanga ama kutoa fidia unaotekelezwa na Halmashauri ya Bandari, hadi pale mpango unaokubalika na washikadau utakapoundwa,
3. Kuundwa kwa mpango mzuri wa kuregesha upya mazingira ya bahari yatakayo athiriwa,
4. Kujumuishwa kwa wadau wote muhimu katika majadiliano ya kutatua mzozo,
5. Kuundwa kwa kamati ya pamoja ya kufuatizia na kutathmini mathara ya oparesheni ya kuvuna mchanga baharini.

Mapendekezo haya yalijadiliwa katika mikutano iliyofanyika Mei 16, 2019, kati ya wawakilishi wa KCNRRN, Serikali ya Kaunti ya Kwale, NECSA-K na wawakilishi wa Serekali ya Kitaifa. Wawakilishi waliweza kukutana na Bw.

Katika mikutano yote miwili, mawaziri waliwahakikishia kuwa wako mbioni kutafuta suluhu.

Kufikia katikati ya Juni 2019, KCNRRN, pamoja na shirika la Wakaazi wa Kusini mwa Pwani (SCRA) waliwasilisha kesi kotini



Bw. Salim Athman, Katibu wa Utalii, alipofanya mkutano na wawakilishi wa KCNRRN, Serikali ya Kaunti ya Kwale na NECSA-K ofisini kwake.

Chris Obure, Katibu Msimamizi Katika Wizara ya Usafiri, Miundombinu, Nyumba na Maendeleo ya Miji, na Bw. Salim Athman, Katibu wa Utalii katika Wizara ya Utalii na Wanyamapori, katika ofisi zao mjini Nairobi.

kumzuia Waziri wa Usafiri, Miundombinu, Nyumba na Maendeleo ya Miji, pamoja na Halmashauri ya Bandari, kutovuna ama kutupa tope katika pwani ya Likoni hadi Diani. Kesi hii itasikizwa tarehe 29 Mei 2019.



Bw. Omar Abdalla Juma (kushoto), Katibu, Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Wasini, akimuelezea Prof. Micheni Ntiba, Katibu Mkuu katika Wizara ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Soko, mchakato wa kutengeneza bustani ya matumbawe kisiwani Wasini.

SIKU YA MTAFITI BAHARINI

Shirika la Utafiti wa Bahari na Uvuvi la Kenya huandaa Siku ya Mtafiti wa Bahari na Uvuvi kila mwaka kuonyesha shughuli inazotekeleza kuboresha uhifadhi wa bahari na kusaidia chumo riziki za jamii na uchumi kwa ujumla.

Mwaka huu, Siku ya Mtafiti iliadhimishwa katika makao

makuu ya shirika, English Point, Mkomani, Mombasa, tarehe 30 na 31 Mei, 2019.

Kauli mbiu mwaka huu ilikuwa ***“Utafiti kwa Uchumi Baharini na Chakula Toshelezi”***

Bw. Omar Abdalla Juma, Katibu wa Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Wasini, aliwawakilishwa katika sherehe

hizi. Bw. Omar alipata fursa ya kuelezea walio hudhuria kuhusu mchakato wa kuregesha upya matumbawe kisiwani Wasini, Kaunti ya Kwale, kupitia upanzi wa matumbawe.

Shirika la Utafiti wa Bahari na Uvuvi la Kenya limekuwa mshirika wake mkubwa.

Shirika hili lilisaidia kuunda na kutenga hekari 352 za eneo la usimamizi wa pamoja baharini, ikiwemo hekari 30, eneo la uhifadhi (bila uvuvi wowote). Eneo hili la uhifadhi hutumiwa kulinda matumbawe, mazalio ya samaki na kuvutia watalii.

Shirika lilisaidia kwa ujuzi katika mradi wa kuregesha upya maeneo ya matumbawe kisiwani Wasini, na kuwezesha kuregesha upya hekari 15 za eneo la matumbawe.

Mbali na miradi ya kuregesha upya mazingira ya bahari yaliyo haribika, shirika limesaidia kuthibiti athari za mabadiliko ya hali ya hewa kupitia mradi wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Kaboni ya Baharini kwa miaka 15 iliyopita. Mradi huu, maarufu kama Mikoko Pamoja, ni mradi wa jamii ya

Gazi, Kaunti ya Kwale. Mikoko Pamoja unalenga kulinda mikoko na maeneo yake, pamoja na kuunganisha jamii na soko la hewa mkaa.

Katika miradi ya kutosheleza chakula na kukuza uchumi, shirika lilishirikiana na mashirika mengine ya



Matumbawe ya kupendeza kisiwani Wasini.

kiserikali, chini ya mwavuli wa Kamati Tekelezi ya Uchumi Baharini, kusaidia ukuzaji wa mwani. Shirika linaaidia Wakulima wa Mwani wa Kibuyuni, chini ya Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Kibuyuni, kwa ujuzi na kukuza biashara ya mwani. Wakulima wa Mwani wa Kibuyuni, kupitia usaidizi

huu, wameweza kuzalisha sabuni za kuoga, sabuni za kufulia na sabuni za kuoshea nywele kutoka kwa mwani.

Mazingira ya bahari yameendelea kuzorota ijapo kuwa kuna miradi kadhaa ya kuboresha mazingira. Tope, kilimo bila mpangilio, maendeleo kanda ya pwani bila mpango, uvuvi kupita kiasi, matumizi ya vifaa haramu vya uvuvi, uharibifu wa mimea pwani, hasa mikoko, na uchafuzi ni baadhi ya tisho kwa mazingira ya bahari.

Ina aminika kuwa 90% ya uchafu jijini Mombasa, ikiwemo plastiki na maji taka, huelekea baharini.

Uchafuzi, haumalizi tu viumbe hai baharini, bali pia hupunguza ubora wa bidhaa za uchumi baharini.

Wazo la kuandaa na kusherehekea Siku ya Kasa Duniani lilianzishwa na shirika la Marekani la Kuokoa Kobe. Nia yao kuu ilikuwa kutambulisha, kuongeza ufahamu, na heshima kwa kasa na kobe, na kuhimiza jamii kusaidia kasa na kobe kuishi na kustawi.

Shirika la Marekani la Kuokoa Kobe liliandaa na kufadhili sherehe za kwanza za Siku ya Kasa Duniani tarehe 23 Mei 2000, na siku hii imekuwa ikisherehekewa kila mwaka

kasa. Umma, na hasa Watoto wa shule, wanaweza kuandaa shughuli ya kusafisha fuo na maeneo ya kuzalia kasa, na kuambatanisha na hotuba zilizo jaa hamasa kuhusu kasa na kobe.

Kuna aina saba za kasa duniani. Aina hizi ni Ng'amba (Hawksbills, hatari kubwa ya kuangamia), Kijivujivu (Kemp's Rيدleys, hatari kubwa ya kuangamia), Kasa wa Kawaida (Greens, hatari ya kuangamia),



Kasa wa Kawaida (Green Turtle)

- uepuke kasa wanaotaga ama kuangua,
4. Punguza chemikali unazotumia,
 5. Jitolee katika shughuli za kulinda na kuongeza

TUSHEREHEKEE KASA DUNIANI!

duniani kote.

Kuvaa nguo mfano wa kasa, kuokoa kasa walioshikwa na nyavu, na utafiti wa kasa, ni baadhi ya shughuli zinazofanywa siku hii kusherehekea



Kasa Ng'amba (Hawksbill Turtle)

Ngozi (Leatherbacks, hatarini), Duvi (Loggerheads, hatarini), Kasa (Olive Rيدleys, hatarini) na Bapa (Flatbacks, hakuna habari kamilifu).

Tunawezaje Kulinda Kasa?

1. Zima taa zinazo onekana kutoka ufuoni!
2. Punguza taka unazozalisha na usaidie kusafisha taka unazoziona ufuoni,
3. Tambua maeneo ya mazalio ya kasa na

nafasi za kasa kuishi!



Bi Janet Mueni (Muandishi wa Makala) hufanya kazi katika Ofisi ya Watu Mazingira Ulimwenguni.

TUZO ZA WASINI!

Robo ya pili ya 2019 imekuwa msimu wa kutambuliwa kwa juhudi za Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Wasini. Kikundi hiki cha kijamii kinasimamia kituo cha kupokea samaki cha kijiji cha Wasini na rasili mali za bahari zinazo zunguka kituo hicho

Tuzo kwa kikundi hiki zilianza kupokewa Mei 2019 kwa kwa Tuzo la Utalii Endelevu Afrika, moja ya mpango wa kutuza vikundi na mashirika ya utalii katika Kongamano la Utalii Endelevu Afrika. Kongamano hili la kila mwaka huleta pamoja washikadau kujadili na kubadilishana habari na maarifa kuhusu utalii endelevu, na kujenga mitandao ya uhusiano. Kongamano la 2019 ni la tano na huandaliwa na shirika la Sustainable Travel and Tourism Agenda. Kongamano lilifanyika mjini Mombasa, Kenya.

Kauli mbiu ya 2019 ilikuwa Utalii Endelevu kwa Bahari Endelevu. Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Wasini kilikuwa cha pili katika kitengo cha Ulinzi Bunifu wa Maisha Baharini (Uhifadhi wa Viumbe na Mazingira).

Sherehe za Siku ya Wafanyikazi wa Umma Afrika husherehekewa kila mwaka kutambua thamani na fadhila za utumishi kwa jamii. Sherehe za 2019 ziliandaliwa nchini Kenya, kuanzia tarehe 21 hadi 23 Juni, katika jumba la mikutani ya kimataifa, Kenya International Conference Centre, Nairobi. Sherehe za 2019 ni za saba, na ziliongozwa na Wizara ya Huduma za Umma, Jinsia na Vijana. Sherehe hizi pia hutoa fursa ya kutafakari jinsi huduma kwa umma inasaidia kukuza uchumi na maendeleo barani.

Kauli mbiu ya 2019 ilikuwa Muingiliano kati ya Kujenga Uwezo wa Vijana na Uhamiaji: Kuimarisha Utawala Bora, Teknolojia ya

Mawasiliano na Uvumbuzi kwa Huduma Bora kwa wote. Kulikuwa na maonyesho ya uvumbuzi na kasi ya maendeleo barani Afrika.

Ni katika sherehe hizi ambapo Kikundi cha Usimamizi wa Fuo ya Wasini kilijishindia tuzo



Bw. Abubakar Ahmed, muandishi wa makala, apokea tuzo kwa niaba ya kikundi.

mbili kwa mradi bunifu wa kuregesha upya matumbawe katika kisiwa cha Wasini. Walipata Tuzo ya Kwanza katika kitengo cha Uvumbuzi Wenye Matumaini Makubwa nchini Kenya na kupata Tuzo ya Pili katika kitengo hicho barani Afrika.

UTALII WA NYUMBANI

KAMBI YA PLOVER, NI NYUMBANI MBALI NA NYUMBANI.



Bw. Wachira Ruhiu, mmiliki na meneja, Kambi ya Plover na Utalii Nyumbani.

Kambi ya Plover inapatikana katika uwanda wa Kinangop, ulio kati ya Bonde la Ufa, kwa upande wa magharibi, na Milima ya Aberdare, kwa upande wa mashariki. Uwanda wa Kinangop umechukua hekari 77,000, na ni hapa ambapo Tokeo wa Sharpe (Sharpe's Longclaw), ndege wa mbuga za nyasi ambao wako katika hatari ya kuangamia, wanapatikana peke yake ulimwenguni kote.

Utalii nyumbani umeanza kupata umaarufu katika siku za hivi karibuni, kama mahali pa mapumziko na kulala kwa watalii katika makao ya mwenyeji wao. Umaarufu wa utalii nyumbani kama mahali mbadala kwa watalii ni kutokana na urahisi ambao watalii wa muda mrefu wanapata ikilinganishwa na hoteli, na mapokezi maalum ambayo hupatikana tu katika mazingira ya nyumbani.

Bw. Wachira Kariuki, alianzisha Kambi ya Plover, iliyoko Murungaru, Kaunti ya Nyandarua, Kenya, January 2012. Kambi hii ambayo imekuwa maarufu kwa utalii nyumbani, inatoa huduma za kupiga kambi na za utalii nyumbani kwa watalii wa humu nchini na wa kimataifa.



Bustani katika Kambi ya Plover ina viti vilivyo tengenezwa kwa vifaa kutoka mtaani.



Shughuli mbalimbali hufanywa hapa ikiwemo sherehe za harusi, maadhimisho ya siku za kuzaliwa na tamasha nyinginezo.

Bw. Wachira ameweza kutoa huduma mbalimbali za kambi na utalii nyumbani kutokana na vivutio vya makao na mazingira vinavyoptatikana katika eneo hili. Kambi ya Plover inatoa huduma zifuatazo: -

1. Utalii kwa sehemu za ki-historia kama vile mapango ya wapigania uhuru wa Mau Mau, na makazi ya zamani ya wakoloni,
2. Utalii Mazingira kwa wapenzi wa ndege wanao patikana katika mbuga za nyasi za Kinangop, misitu na maeneo lowevu,

- ikiwemo Ziwa Ol Bolossat. Kambi ya Plover pia huandaa safari za kujivinjari, safari kwa miguu na hata mazoezi ya kujenga uhusiano bora wa wafanyikazi katika maeneo ya Bonde la Ufa na Milima ya Aberdare,
3. Utalii wa Tamaduni kwa wale ambao wangependa mwonjo wa mila na tamaduni za Agikuyu. Kuna makao, makavazi ya kitamaduni na wacheza ngoma za kiasili,
4. Elimu ya Mazingira na Uhifadhi kwa wanafunzi na watafiti, na,

Watu Mazingira, Ulimwengu!

5. Watalii wa Kilimo kwa watalii ambao wangependa kuona na kujifunza ukulima endelevu na kuona maisha ya mkulima katika eneo hili.

Kambi ya Plover imeweza kutambuliwa na Wizara ya utalii ya Serikali ya Kaunti ya Nyandarua kama kituo muhimu cha utalii mazingira na utalii nyumbani, na kwa juhudi zake za kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi mazingira na tamaduni za jamii ya Agikuyu.

KARIBUNI NYUMBANI!

Mtandao wetu wa Watu Mazingira Ulimwenguni umeendelea kukua. Vijana, katika robo hii ya mwaka, wamejiunga nasi kwa wingi. Kwa ujumla, vijana 22, kutoka Kenya na Zimbabwe, walijisajili kwa mtandao na kufikisha 24 idadi ya wanachama walio sajiliwa robo hii. Kwa mara ya kwanza tumeweza kuandikisha Klabu ya Vijana. Klabu ya Vijana Wanamazingira ya Shule ya Msingi ya Utange, Kaunti ya Mombasa, Kenya, ilisajili wanachama 20.

Kwa hivyo, ni furaha yetu kuwajulisha na kuwakaribisha nyumbani wanachama wetu wanya.

1. Mariam Hamisi (Taveta, Kenya),
2. Nakamyuka Olivia (Jinja, Uganda),
3. Jayden Tabengwa (Bulawayo, Zimbabwe),
4. Jaysen Tabengwa (Bulawayo, Zimbabwe),
5. Joyce Mwagandi (Utange, Kenya),
6. Salim Omar (Utange, Kenya),
7. Baraka Kidaya (Utange, Kenya),
8. Rooney Ojuka (Utange, Kenya),
9. Beatrice Mengi (Utange, Kenya),
10. Halima Mwajuma (Utange, Kenya),
11. Mary Mwamuye (Utange, Kenya),
12. Dranis Atieno (Utange, Kenya),
13. Ann Wangui (Utange, Kenya),
14. Zawadi Kadzo Utange, Kenya),
15. Purity Isaac (Utange, Kenya),
16. Mercy Gedion (Utange, Kenya),
17. Sauda said (Utange, Kenya),
18. Hyna Monday (Utange, Kenya),
19. Happy Juma (Utange, Kenya),
20. Paul Mwambire (Utange, Kenya),
21. Fauzia Ramadhan (Mombasa, Kenya),
22. Faith Furaha (Mombasa, Kenya),
23. Zainab Suleiman (Mombasa, Kenya),
24. Tatu Kassim (Mombasa, Kenya).



Nakamyuka Olivia, Jijini Jinja, Uganda.



Matumizi yasiyo endelevu, pamoja na athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ina hatarisha mazingira na mali asili ulimwenguni. Kwa njia moja ama nyingine, tunajaribu kubadilisha hali hii kwa kuchangia kuwepo kwa matumizi bora ya mali asili iliyobaki na kuhakikisha maisha yanaendelea.

Lakini kuna kundi la wana mazingira ambao wamechukua sheria mikononi mwao kuona kuwa mazingira yanalindwa.

Kutana naye Bi. Paige Samblanet (kushoto), P4N-349, kutoka California, Marekani. Bi. Paige ni mwanafunzi akiwa mwaka wa tatu, akisomea sheria ya mazingira, kawi na maji. Yeye ni mwanachama wa Wanasheria wa California na amefanya kazi na mashirika kama vile EarthJustice na Jopo la Kawi la California.

Mnamo 2014, Bi. Paige alikuwa nchini Kenya kwa miezi 6 na kufanya kazi na shirika la Global Vision International (GVI). Akiwa Kenya, aliweza pia kujifunza mengi kuhusu wanyama pori na kufunza katika shule za Kisiwa cha Wasini na eneo la Shimoni.

KAMATI KUU (SUMMIT)

1. Silvanus Uunona – Mwenyekiti,
2. Yaa Tiwah – Mwenyekiti Mwenza,
3. Moses Ziro – Katibu,
4. Frank Maro – Mweka Hazina,
5. Phathisani Tabengwa – Mwanachama,
6. Cheli Gurung – Mwanachama,
7. Nancy Saumu Ronald – Mwanachama,
8. Emma Kyomukama – Mwanachama.

JARIDA LA WATU MAZINGIRA

1. Phathisani Tabengwa - Mhariri.
2. Catherine Musili - Mhariri Mwenza.

ANUANI YA OFISI

Mtaa wa Vescon 1, Nyumba No. 199,
Barabara ya Felix Bunche, Bamburi,
MOMBASA-KENYA.

ANUANI YA BARUA

Watu Mazingira Ulimwenguni,
c/o Africa Nature Organization,
SLP 2227-80100,
MOMBASA-KENYA.

MAJUKWAA

Maji

Mshirikishi: Silvanus Uunona (Namibia),
Mshirikishi Mwenza: Soledad Castro (Costa Rica).

Wanyama Pori na Misit

Mshirikishi: Nancy Saumu Ronald (Kenya),
Mshirikishi Mwenza: Dorothy Syallow (Kenya).

Kilimo Hifadhi na Uvuvi

Mshirikishi: Yaa Tiwah (Ghana),
Mshirikishi Mwenza: Setondji Gaston (Gabon).

Elimu Mazingira na Hamasisho

Mshirikishi: Phathisani Tabengwa (Zimbabwe),
Mshirikishi Mwenza: Zelalem Abera (Ethiopia).

Vijana

Mshirikishi: Cheli Gurung (Nepal),
Mshirikishi Mwenza: Raymond Mwambire (Kenya).

Jamii Asili

Mshirikishi: Moses Ziro (Kenya),
Mshirikishi Mwenza: Jazzy Razalojaona (Madagascar).

Wanawake

Mshirikishi: Emma Kyomukama (Uganda),
Mshirikishi Mwenza: Ashengai Kimath (Tanzania).

Biashara Mazingira

Mshirikishi: Frank Maro (Tanzania),
Mshirikishi Mwenza: Fadhila Ghikas (Kenya).

